LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Block 44, Plot 508 & 509, Kijitonyama,
P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA • Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037,
E-mail: lhrc@humanrights.or.tz Website: www.humanrights.or.tz

for a Just and Equitable Society

TAMKO KWA VYOMBO VYA HABARI KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA KUPINGA ADHABU YA KIFO DUNIANI, TAREHE 10/10/2014

Ndugu wanahabari,

Leo ni Siku ya Kupinga Adhabu ya Kifo duniani, siku ambayo huadhimishwa kila mwaka tarehe 10/10 ili kushawishi mabadiliko ya katiba, sera, sheria na utekelezaji wake ili kutokomeza adhabu ya kifo. Adhabu hii inaondoa Haki ya Kuishi ambayo ni haki ya msingi ya binadamu. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kwa muda mrefu tangu kuanzishwa kwake kimekuwa kikipigania na kufuatilia masuala mbalimbali yanayotokana na vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu hapa nchini ikiwemo kushinikiza ufutwaji wa adhabu hii.

Kituo katika kuadhimisha siku hii ya kupinga adhabu ya kifo duniani, yenye kauli mbiu ya "***Ugonjwa wa akili sio kosa - watunzwe sio kuuwawa***"kauli mbiu hii inakumbusha juu ya hatari inayoweza kutokea kwa watu walio na ugonjwa wa akili kutuhumiwa na kuhukumiwa kifo au adhabu hii kutekelezwa dhidi yao.Kulingana na changamoto walizonazo ambazo zinaweza kuwafanya washindwe kujitetea au kushiriki kikamilifu kwenye mashitaka dhidi yao.

Hivyo basi, katika siku hii muhimu kote Duniani, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinaungana na watu na wadau wengine wanaotetea haki za Binadamu duniani kote kupinga adhabu hii ambayo inakiuka haki ya kuishi kama inavyoainishwa na Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 ambayo inaeleza wazi katika;

Ibara ya 14:
Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake, kwa mujibu wa sheria"

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa baadhi ya nchi chache duniani (kama vile China, Iran, Korea Kaskazini na Marekani) ambazo bado zinaruhusu na kutekeleza adhabu ya kifo katika sheria zao. Nchini Tanzania adhabu ya kifo ipo kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania, kifungu cha 197 kinachoeleza kwamba;

Mtu yeyote aliyepatikana na hatia ya kuua, atahukumiwa adhabu ya kifo.

Pia adhabu ya kifo imewekwa kama adhabu kwa makosa ya uhaini na makosa mengine ya kijeshi. Japo kuwa kwa miaka 20 sasa haijatekelezwa hapa nchini wakati watu wengi wameendelea kuhukumiwa adhabu hii kwa makosa ya mauaji na mengineyo kama yalivyoainishwa kwa mujibu wa sheria.

Board of Directors:
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - *Chairperson*, Ms. Athanasia Soka (Adv) - *Vice Chairperson*, Dr. Helen Kijo-Bisimba - *Secretary*, Mr. Francis Stolla (Adv), Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Ms. Maria Sarungi Tsehai, Ms. Diana Monica Kisaka, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya.

Licha ya kampeni na umuhimu wa kufuta adhabu ya kifo bado tumeona kuwa adhabu hii ya kifo imeendelea kuwepo katika Katiba iliyopendekezwa ambayo imepitishwa na Bunge la Katiba hivi karibuni. Katika katiba hii pendekezwa Ibara ya 33 inasema

Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake kutoka katika serikali na jamii kwa mujibu wa sheria za nchi".

Pia katika Ibara ya 95(1) (c) iimempa Rais mamlaka ya kubadilisha adhabu ya kifo kuwa adhabu ya kifungo cha maisha.

Kwa maana hiyo bado katiba hii pendekezwa inaendeleza uwepo wa adhabu ya kifo kikatiba ambayo ni kinyume na haki za binadamu, katika karne hii ambayo nchi nyingi zimefuta adhabu hii. Fursa ya kufuta adhabu ya kifo ilipatikana katika mchakato wa uandaaji wa katiba mpya na tunaona ipo haja kabisa kutopoteza fursa hii.

Pamoja na hilo ipo haja ya kujenga uelewa mpana kwa wanajamii na viongozi kuwa kampeni hii ya kupinga adhabu ya kifo,haina maana kwamba tunatetea wauaji au matendo ya mauaji kuendelea kwa mfano mauaji ya watu wenye ualbino. Msukumo ni kuwa uhai unathamani kubwa na hautakiwi kuondolewa na mtu yeyote au chombo chochote. Hivyo kumuuwa mtu aliye uwa sio njia sahihi ya kukabili makosa hayo wala kuzuia utendwaji wa kosa kama hilo bali ni njia ya kulipiza kisasi na haitofautishi baina ya mtenda kosa la mauaji na mtekeleza adhabu ya kifo.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapinga utekelezwaji na uwepo wa adhabu hii kwenye katiba na sheria za nchi, kwani adhabu hii pamoja na kwamba inakiuka haki ya kuishi lakini pia ikumbukwe kwamba;

i. **Hakuna nchi** yenye haki ya kuchukua au kukatisha maisha ya raia wake;

ii. Adhabu ya kifo **haiweki jamii katika hali ya usalama:** Kamwe haijawahi kuonyesha kuwa adhabu ya kifo inazuia kabisa uhalifu kutendeka zaidi kuliko adhabu nyingine;

iii. Adhabu ya kifo **Haina usawa:** Adhabu ya kifo ni ya kibaguzi na mara nyingi hutumika vibaya dhidi ya maskini, wenye ugonjwa wa akili, watu kutoka makundi yaliyo pembezoni, na katika maeneo mengine duniani, sababu ya ubaguzi wa dini na jinsia;

iv. Adhabu ya Kifo **Hairekebishiki:** Hakuna Mfumo wa utoaji haki usiokua na makosa ya kisheria na/au Kimahakama. Kwa hiyo watu wema, wasiokua na hatia wanaweza kuhukumiwa kifo kimakosa na kisha kushindwa kurudisha uhai wao pindi adhabu hii itakapotekelezwa.

v. Adhabu ya kifo **sio ya kibinadamu, ni ya kikatili na ya udhalilishaji:** Hali ya kusubiri kunyongwa inasababisha matatizo makubwa ya kisaikolojia na utekelezaji wake ni wa kinyama;

Board of Directors:
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - *Chairperson*, Ms. Athanasia Soka (Adv) - *Vice Chairperson*, Dr. Helen Kijo-Bisimba - *Secretary*, Mr. Francis Stolla (Adv), Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Ms. Maria Sarungi Tsehai, Ms. Diana Monica Kisaka, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya.

vi. **Hutumiwa vibaya sana na inakiuka viwango vya kimataifa:** Adhabu ya kifo inavunja misingi ya Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la mwaka 1948 ambalo linasema kila mtu ana haki ya kuishi, na pia ni marufuku kutoa adhabu ya kikatili inayotweza utu. Pia inapingana na mwenendo/mtazamo wa kimataifa juu ya ufutwaji wa adhabu ya kifo kutokana na kura 3 katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, likitaka kuanzishwa kwa uzuiaji wa adhabu ya kifo (Mapendekezo 62/149, 63/168,65/206 na 67/176 yaliyoridhiwa mnamo Disemba 2007,2008,2010 na 2012);

vii. Adhabu ya kifo inaondoa uwezekano wowote wa mkosaji kuweza kujirekebisha pindi inapokuwa imetekelezwa.

Hivyo, katika kuadhimisha siku hii ya leo tarehe 10/10/2014, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinashauri mambo yafuatayo;

1. Ibara ya 33 ya katiba pendekezwa kufuta na kuondoa kabisa neno ***kwa mujibu wa sheria*** za ***nchi*** ilikuhakikisha kuwa haki ya kuishi inakuwepo bila kipingamizi au kuminywa na sheria yoyote.

2. Pia kuondoa Ibara ya 95 (1) (c) ya Katiba Pendekezwa inayompa Raisi mamlaka ya kubadilisha utekelezwaji wa adhabu hii. Hivyo Ibara hii ifutwe kuwezesha Katiba ijayo kufuta kabisa adhabu ya kifo na si kuibadilisha .Hii ni kutokana na adhabu hii kushindwa kukomesha au kuondoa kabisa makosa yanayo hukumiwa adhabu hiyo.

3. Sheria ya Kanuni ya Adhabu inatakiwa kubadilishwa na kufuta kabisa adhabu ya kifo na kutoa adhabu mbadala kama kifungo cha maisha na kazi ngumu kwa watuhumiwa wa mauaji ili kulinda haki hii ya msingi.

4. Tanzania inapaswa kujifunza kutoka nchi nyingine duniani ambazo hazitekelezi adhabu ya kifo ni kwa jinsi gani zimekuwa zikishughulikia watu wenye makosa ya kuua;

5. Kwa pamoja wananchi wa Tanzania tuikatae adhabu ya kifo, tusikubali kuwa wauuaji.

Asanteni kwa kunisikiliza,

Dkt. Helen Kijo-Bisimba
Mkurugenzi Mtendaji

Board of Directors: